OFISI YA RAIS-TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO

ANUANI YA SIMU
SIMU: +255 (0)765 759 879
BARUA PEPE:
mlowass2014@gmail.com



SHULE YA SEKONDARI MLOWA,
S. L. P 12,
MAKAMBAKO.

18.12.2020

KUMB.NA.ML.SS/AD 2020/VOL.1/08
JINA LA MWANAFUNZI. ……
SHULE ALIYOTOKA. ……..
MJI: MAKAMBAKO.

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KWA MWANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA 2021

1: UTANGULIZI.

Uongozi wa shule ya sekondari Mlowa, unachukua nafsi hii kukujulisha kuwa wewe ni miongoni mwa watahiniwa wachache wa darasa la saba (7) 2020 mkoani Njombe waliofaulu na kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii.

Pamoja na kukupongeza kwa kupata nafasi hiyo adimu, huna budi kuonesha kwa vitendo vya wazi kuwa unaijali na kuitumia vizuri nafasi hii kwa manufaa yako bunafsi, jamii na Taifa kwa ujumla.

Utakapokuwa hapa shuleni, utakuwa na wajibu wa kusoma kwa bidii, kutii na kufuata sheria za shule, kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za kielimu shuleni kama michezo, usafi, kazi za mikono na kuishi kwa amani, upendo na ushirikiano na wanfunzi wenzako na watumishi wa shule hii ili uweze kupata elimu bora kwa maisha endelevu.

2: MAELEZO KUHUSU SHULE

Shule ya sekondari Mlowa ni shule ya kutwa na ya mchanganyiko (wavulana na wasichana). Shule ipo Kata ya Mlowa, Tarafa ya Makambako katika Halmashauri ya Mji wa Makambako. Shule hii ni ya umma (siyo ya binafsi), na inayoendeshwa na wazazi wakishirikiana na Halmashauri ya Mji wa Makambako.

Shule ya Sekondari Mlowa iko mashariki mwa mji wa Makambako umbali wa kilomita 10 kutoka stendi kuu ya mabasi na inafikika kupitia barabara iendayo Mahongole/Kifumbe kupitia Shule ya Msingi Uhuru.

3: VIAMBATANISHO

- **a)** Fomu ya mahitaji na michango ya shule (**FOMU A**)
- **b)** Fomu ya maelekezo binafsi yahusuyo mwanafunzi (**FOMU B**)
- **c)** Fomu ya hali afya ya mwanafunzi
- **d)** Sheria za shule

Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 mwanafunzi afike na mzazi au mlezi wake kuanzia saa 1:30 asubuhi.

4: MUHIMU:

A. Sare ziwe za kitambaa sahihi, zisizobana, zisiwe fupi, na zishonwe mishono sahihi.

B. Tafadhali jaza kwa usahihi taarifa binafsi za mwanafunzi pamoja na anwani ya makazi na namba za simu.

C. Mzazi/mlezi na mwanafunzi msome kwa makini sheria/kanuni za shule na kuzielewa ili kumsaidia mwanafunzi awapo shule kuwa na nidhamu na kupata kinachotarajiwa na mzazi/mlezi, jamii na Taifa kwa ujumla. Hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya Mwanafunzi yeyote ambaye hatafuata sheria/kanuni za shule

D. Mzazi/mlezi mpeleke mwanafunzi kwa Mganga Mkuu wa kituo cha afya au Hospitali ya Wilaya ili apimwe na kujaziwa fomu ya afya iliyoambatanishwa, itasainiwa na kuwekwa muhuri.

Zingatia: Fomu hiyo lazima ijazwe na vituo vya afya vya Serikali na Hospitali za Serikali, na Linda afya ya mwanafunzi kwa kutoa taarifa sahihi

E. Mzazi/mlezi mwandalie mtoto wako **CHETI CHA KUZALIWA** ili kimsaidia kwenye masomo ya juu lakini pia kuwa na kumbukumbu sahihi za kuzaliwa kwa mwanafunzi pale taarifa hizo zinapohitajika

Asante na hongera sana
Ni mimi katika malezi ya vijana

_____

R.I. KYANDO
MKUU WA SHULE
0766374719

FOMU A: MAHITAJI YA SHULE

MLOWA SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 12, MAKAMBAKO
EDUCATION IS A BEACON OF HOPE
"YOU WILL NEVER WALK ALONE"

(a).Michango ya vifaa na chakula

Na	WAVULANA	Idadi	WASICHANA	Idadi
1	Suruali mifuko mitatu rangi ya kijani bluu (Benjamin Mkapa)	02	Suruali mifuko miwili ya mbele rangi ya kijani bluu (Benjamin Mkapa)	02
2	Mashati meupe mikono mirefu	02	Gauni lenye mikono mirefu na kola lenye urefu juu ya goti, kitambaa cheupe. (koshibo)	02
3	Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba (kisigino kifupi)	02	Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba (kisigino kifupi)	02
4	Tracksuit nyeusi Adidas	01	Tracksuit rangi ya light blue Adidas	
5	Soksi fupi nyeusi	02	Soksi ndefu nyeupe (stockings)	02
6	Sweta rangi ya damu ya mzee	02	Sweta rangi ya damu ya mzee	02
7	Madaftari ya mazoezi aina ya A-12	12	Madaftari ya mazoezi aina ya A-12	12
8	Mkebe wa Hisabati	01	Mkebe wa hisabati	01
9	Rula ft 1 (ya kioo/plastics)	01	Rula ft 1 (ya kioo/plastics)	01
10	Kalamu za wino bluu/nyeusi	02	Kalamu za wino bluu/nyeusi	02
11	Penseli na mfuto	01	Penseli na mfuto	01
12	Oxford English dictionary	01	Oxford English dictionary	01
13	File (spiral file)	01	File (spiral file)	01
14	Ndoo ndogo	01	Ndoo ndogo	01
15	Kwanja (Slasher) na Panga	01	Jembe na mpini wake	01
16	**Mchango wa chakula** i). Mahindi kilo 40 (debe 2) ii). Maharage kilo 20 (debe 1) iii). Fedha tsh. 30,000/= Kwa mwaka fedha inalipwa kwa awamu mbili katika akaunti ya shule Jina la akaunti: **Mlowa Secondary School EK.** Namba ya akaunti: **60310018875** Jina la benki: NMB		**Mchango wa chakula** i). Mahindi kilo 40 (debe 2) ii). Maharage kilo 20 (debe 1) iii). Fedha tsh. 30,000/= Kwa mwaka fedha inalipwa kwa awamu mbili katika akaunti ya shule Jina la akaunti: **Mlowa Secondary School EK.** Namba ya akaunti: **60310018875** Jina la benki: NMB	

MUHIMU:i) Ni muhimu vifaa vyote viletwe kwani vitamsaidia mwanafunzi katika usomaji

ii). Ni lazima kila mwanafunzi awe na sare za shule mbili mbili kadri ilivyo kwenye jedwali na siku ya kuripoti tutakagua na aje nazo zote.

iii). Mchango wa chakula unalipwa kwa awamu mbili na unalipwa benki tu kwa akaunti iliyoneshwa kwenye jedwali hapo juu.

PRESIDENT'S OFFICE - RALG
MAKAMBAKO TOWN COUNCI

MLOWA SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 12 ,
MAKAMBAKO.

REF.NO: ML.SS/AD/2020/08. 18/12/2020

THE MEDICAL OFFICER
_____
_____
_____

REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Kindly examine (Name)_____ to determine her/his physical and mental fitness to pursue secondary school studies.

_____
RAYMOND I. KYANDO.
THE HEADMASTER

1. Eyesight _____
2. Hearing _____
3. Speech_____
4. Limb _____
5. Leprosy _____
6. Epilepsy _____
7. Cardiac diseases _____
8. Rheumatism _____
9. Venereal _____
10. Pregnancy (for girls)_____
11. Any other serious disease _____
12. Any disabilities _____

General comments _____
_____
_____
_____

Name _____ Signature _____

Designation _____

Stamp

Date _____

SARE YA SHULE YA WANAFUNZI WA KIKE (WASICHANA)

D: **SHERIA ZA SHULE**

1. Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara tu anapowasili shuleni;
   (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
   (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli(shughuli za kitaaluma na shughuli za nje).
   (c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni(Evening Preparation).
   (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
   (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka ya shulewakati wote wa uanafunzi wako.
   (f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
   (g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapokuwa shuleni(nguo zingine nje ya sare / maagizo ya shule haziruhusiwi).
   (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
   (i) Lugha chafu, matusi,ugomvi,fitina,kupiga/kupigana ni mwiko kabisa.
   (j) Unywaji wa vileo,kuuza pombe na uvutaji wa aina yoyote ni mwiko kwa wanafunzi.
   (k) Wizi wa aina yoyote ni mwiko kwa mwanafunzi.
   (l) Uharibifu na upotevu wa mali binafsi na mali ya umma ni kosa kubwa.
   (m) Mwanafunzi haruhusiwi kuoa au kuolewa akiwa bado mwanafunzi. Akibainika atafukuzwa shule mara moja,aidha ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na mahusiano/uhusiano wa kimapenzi.Akibainika adhabu yake ni kufukuzwa shule.
   (n) Wageni wataruhusiwa kuwaona/kuonana na wanafunzi baada ya kujitambulisha na kupokelewa na mwalimu wa zamu,kila Jumapili ya kwanza ya mwezi.
   (o) Ni mwiko kwa mwanafunzi yoyote kwenda nyumba za walimu na wafanyakazi bila ruhusa ya pekee kutoka kwa mwalimu mlezi.
   (p) Ni marufuku kwa Mwafunzi kuwa na simu ya mkononi.

(q) Mgomo wa aina yoyote shuleni ni marufuku na haramu.

(r) Mwanafunzi atafuata maelekezo yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.

(s) Mwanafunzi atajisafirisha mwenyewe wakati wa likizo au pale atakaporudishwa nyumbani/kufukuzwa shule.

2. **Makosa yafuatayo yatasababisha mwanafunzi afukuzwe shule;**

(a) Wizi

(b) Uasherati,ushoga ,ubakaji, kuoa au kuolewa

(c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama cocaine,kubeli n,k

(d) Uvutaji wa sigara

(e) Kupiga au kupigana kwa mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule

(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

(g) Kudharau bendera ya Taifa

(h) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako,walimu au walezi na jamii kwa ujumla

(i) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu

(j) Kukataa adhabu kwa makusudi

(k) Kumiliki **SIMU YA MKONONI** shuleni au vifaa vyovyote vile vinanavyohusiana na simu kama vile betri ya simu, kadi n.k

(l) Kushiriki au kuendeleza imani za kishirikina

(m) Kunyanyapaa au uonevu wa aina yoyote

(n) Kuweka mimba au kupata mimba

(o) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro

(p) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

(q) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kama kunywa sumu n.k

HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO
SHULE YA SEKONDARI MLOWA

FOMU B: MAELEZO BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI

A: 1. Jina la mwanafunzi……..…….

2. Tarehe ya kuzaliwa…….……...

3. Mahali alipozaliwa (wilaya)……mkoa……

B: 1. Baba mzima?.....ndiyo/hapana

2. Mama mzima?..……..…… ndiyo/hapana

C; 1. Jina lamzazi/mlezi anayekulea…….……..

2. Kazi ya mzazi/mlezi…….……..

3. Anuani ya mzazi/mlezi…….……..

4. Namba ya simu: ……..……..……..

5. Mahali ambapo mzazi/mlezi anaishi…….…….

kijiji/mtaa……..… wilaya……..……. Mkoa…….……

D: majina na anuani ya ndugu wengine wa karibu

wanaohusika na malezi ya mwanafunzi huyo.

1. Jina……. Uhusiano…….simu……
2. Jina…….. Uhusiano…….simu……
3. Jina……. Uhusiano…….simu……

E: taarifa za serikali ya mtaa au kata ambako mwanafunzi anatoka.

Jina na sahihi ya kiongozi…….…….

Kata/Mtaa wa ……..……..

Anuani ……..…… simu:……..

SHULE YA SKONDARI MLOWA
MAHITAJI MUHIMU KWA MWANAFUNZI WA HOSTEL.2021

A. MICHANGO NA MAHITAJI MUHIMU

a. Mahindi kilo 160 (Debe 08) kwa mwaka
b. Maharage kilo 40 (Debe 02)
c. Mchele supa kilo 20 (Debe 01)
d. Fedha tshs 110,000/= kwa mwaka
e. Sare ya gauni (shamba dress),kitambaa cha gauni rangi ya damu ya mzee ya kuiva (maroon), mshono wa solo refu – 02

MUHIMU: i. michango ya kifedha ilipwe kupitia Benki ya NMB , kwenye akaunti namba 60310018875, Jina Mlowa Secondary School EK.
ii. Michango inalipwa kwa awamu mbili tu, Januari na Julai ya kila mwaka.
iii. Ni vema mwanafunzi akajiunga na huduma ya bima ya afya.

B. MAHITAJI YA MWANAFUNZI

i. Aje na kitabu cha dini yake.
ii. Sahani, bakuli, kikombe na kijiko.
iii. Aje na ndoo ndogo moja kwa matumizi binafsi.
iv. Taulo na ndala kwa ajili ya kuogea.
v. Shuka mbili (2) za rangi ya pink.
vi. Blanketi zito moja rangi yoyote.
vii. Fedha ya matumizi yake (pocket money).
viii. Sanduku la chuma (tranker) lenye kufuli kwa ajili ya kutunzia mali zake.
ix. Aje na kwanja (slasher) moja (1) chelewa na ufagio mlaini kwa ajili ya usafi.
x. Awe na sare zote za shule ikiwa ni pamoja na tracksuit rangi ya light blue na raba kwa ajili ya michezo.
xi. Aje na mahitaji yote ya shule

NB: Mwanafunzi anatakiwa kufuata sheria na taratibu za shule na wizara kama ilivyoainishwa hapo chini

MAMBO YATAKAYOSABABISHA KUFUKUZWA KUKAA HOSTEL.

i. Kuzembea kujisomea (kutofuata ratiba ya kujisomea)
ii. Kuondoka /kulala nje ya hostel bila ruhusa.
iii. Kushindwa kutimiza mahitaji ya hostel
iv. Kusababisha vurugu (kugombana) kusababisha au kushiriki mgomo.
v. Kuharibu samani za hostel (atawajibika kulipa uharibifu aliousababisha)
vi. Kutoka nje ya hostel bila sare iliyokubalika hata kama mwanafunzi anaruhusa.
vii. Kutorudi muda uliopangwa hata kama unaruhusa
viii. Kutotunza usafi wa mwili, mazingira ya hostel na ya shule kwa ujumla.
ix. Lugha chafu mfano matusi.
x. Kupika au kukutwa na chakula hostel
xi. Kupeleka/kukaribisha marafiki ambao si wahusika wa hostel.
xii. Kwenda nyumba za walimu/watumishi wengine wasiyo walimu bila kibali.
xiii. Kukutwa na simu au kifaa chochote kinachohusiana na simu, mfano: Laini, chaja, nk.
xiv. Kuwa na nguo zaidi ya zile zilizopendekezwa.
xv. Kuwa na silaha/ kitu kinachoweza kutumika kama silaha, mfano: Kisu, bisibisi, nyundo, nk.

_____,

_____,

_____,

_____ /_____ /_____.

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI MLOWA,
S.L.P. 12,
MAKAMBAKO.

Ndugu,

YAH: OMBI LA KUKAA HOSTELI KWA MWANAFUNZI

_____
KIDATO CHA _____

Kichwa cha habari hapo juu cha husika.

Mimi _____ mzazi/mlezi wa Mwanafunzi _____. Ninaomba mtoto wangu aweze kukaa hosteli kwa kipindi chote atakacho kuwepo hapo shuleni.Nitafuata masharti yote yaliyowekwa kwaajili ya hostel na shule kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kulipa michango yote inayotakiwa kwa mwanafunzi anayekee hostel kadri ya taratibu zilizowekwa.

Naahidi kufuata masharti yote yaliyowekwa na iwapo nitakwenda kinyume na masharti hayo basi mtoto wangu aondolewe katika orodha ya wanafunzi wakukaa hosteli.

Ndimi

_____

_____
MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

SIMU NA. _____